

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA ISHIRINI NA MBILI**

**09 MEI, 2024**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

**KIKAO CHA ISHIRINI NA MBILI – TAREHE 09 MEI, 2024**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA MAJI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:**

#### **IV. MASWALI YA KAWAIDA:**

##### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

##### **287. MHESHIMIWA NORA WAZIRI MZERU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaajiri Walimu wa kutosha kutokana na ongezeko kubwa la Wanafunzi.

##### **288. MHESHIMIWA DKT. FLORENCE GEORGE SAMIZI (MUHAMBWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga miundombinu ya Shule ya Sekondari Mkugwa ikiwemo Mabweni, Bwalo na Madarasa - Muhambwe.

##### **289. MHESHIMIWA JANEJELLY JAMES NTATE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaajiri Wataalam wa Maabara Shule za Sekondari ili kupunguza mzigo kwa Walimu wa Sayansi kufanya kazi kama Wataalam wa Maabara.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**290. MHESHIMIWA DKT. ANGELINE SYLVESTER LUBALA MABULA (ILEMELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, lini ujenzi wa Kingo za Mto Msuka Ilemela utakamilika ili kuepusha vifo vya mara kwa mara pindi mvua zinaponyesha.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**291. MHESHIMIWA JACQUELINE KAINJA ANDREW (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, nini mpango wa Serikali kuwezesha upatikanaji wa Vitabu Shule za Msingi ambazo zimeanza Mtaala mpya wa Kingereza kuanzia Darasa la Kwanza.

**WIZARA YA MADINI:**

**292. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia Wachimbaji Wadogo wa Madini Wilaya ya Ulanga.

**WIZARA YA UJENZI:**

**293. MHESHIMIWA SALIM ALAUDIN HASHAM (ULANGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Ifakara – Malinyi – Namtumbo – Mahenge Mjini hadi Lupiro kwa kiwango cha lami.

**294. MHESHIMIWA IDDI KASSIM IDDI (MSALALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Solwa hadi Kahama kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA KILIMO:**

**295. MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP MWANYIKA (NJOMBE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itajenga miundombinu ya Umwagiliaji kwenye maeneo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tarafa ya Igominyi - Njombe.



## **WIZARA YA MAJI:**

### **296. MHESHIMIWA BUPE NELSON MWAKANG'ATA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, kuna mpango gani wa kukamilisha Mradi wa Maji kutoka Ziwa Tanganyika na kusambaza katika Mkoa wa Rukwa.

## **V. HOJA ZA SERIKALI:**

### **WAZIRI WA MAJI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**DODOMA**  
**09 MEI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***  
**KATIBU WA BUNGE**